HOTUBA YA PROF. MARK MWANDOSYA (MB) WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI WAKATI WA UFUNGUZI WA MKUTANO WA KWANZA WA MWAKA WA MAAFISA WA MAJI WA MABONDE, HOTELI YA OCEANIC BAY BAGAMOYO
TAREHE 1 APRILI, 2008

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Dkt. Christine Ishengoma (Mb),
Wenyeviti wa Bodi za Maji za Mabonde,
Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mhandisi Christopher Sayi,
Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Kanali Mstaafu Mrengo Serenge,
Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo, Wizara ya Maji na Umwagiliaji,
Washirika wa Maendeleo,
Maafisa wa Maji wa Mabonde,
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana.

1. Utangulizi

Awali ya yote natanguliza shukrani kwa Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na amani, aliyetuwezesha kukutana siku ya leo hapa Bagamoyo.

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa kumkaribisha Naibu Waziri na mimi katika Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Nawashukuru pia kwa kunikaribisha kwenye mkutano huu wa mwaka, wa Maafisa wa Maji wa Mabonde, hapa mjini Bagamoyo. Kabla yakuendelea, nawakaribisha washiriki wote wa mkutano huu. Ninafurahi kusikia kwamba hapa tunao wawakilishi wa washirika wetu katika maendeleo ya sekta ya maji ambao ni:- Benki ya Dunia; Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GTZ); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA); Shirika la Kimataifa la Hifadhi ya Mazingira (IUCN); na Shirika la Dunia la Hifadhi ya Wanyamapori (WWF).

Ndugu Wajumbe, nimeambiwa kwamba mkutano huu wa Maafisa wa Maji wa Mabonde, ni wa kwanza kufanyika tangu Serikali ilipokamilisha mchakato wa kuanzisha Ofisi za Mabonde yote tisa hapa nchini. Hivyo basi, kwa kuhudhuria kwenu mmewezesha historia kuandikwa. Mkutano huu wa kipekee umejengeka katika maudhui yafuatayo:- K**uweka mfumo wa kutathmini maendeleo ya utekelezaji wa usimamizi wa rasilimali za maji nchini.** Mkutano huu utajadili na kufikia makubaliano juu ya mfumo unaofaa wa kutathmini maendeleo ya utekelezaji wa kazi za usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za maji hapa nchini.

Sina shaka kwamba mfumo huo ndio utakuwa msingi utakaoziwezesha Bodi za Maji za Mabonde kufuatilia na kutathmini mara kwa mara na kwa uwazi, matatizo na changamoto zinazokabili utekelezaji wa usimamizi wa rasilimali za maji nchini na kuwa na njia sahihi za kutatua migogoro ili kuhakikisha kwamba rasilimali hii inakuwa endelevu kwa manufaa yetu ya sasa na vizazi vijavyo.

Ndugu Wajumbe, sote tunafahamu ya kuwa nchi yetu imebahatika kuwa na rasilimali nyingi za maji. Hata hivyo rasilimali hizo hazipatikani kwa uwiano ulio sawa katika maeneo yote. Tanzania imebahatika kuwa na mito, maziwa na vile vile hifadhi kubwa ya maji chini ya ardhi. Pamoja na hali hiyo, yapo matatizo yanayosababisha upungufu wa maji katika baadhi ya maeneo kama yalivyoainishwa katika hotuba iliyotangulia.

2. Hifadhi ya Mazingira ya Vyanzo vya maji

Ndugu Wajumbe, tunaelewa kwamba uhaba au uchafuzi wa maji huathiri sekta nyingi na hutishia uendelevu wa rasilimali hii na kuhatarisha uhai wa viumbe vyote. Mfano dhahiri ni ule wa ukame wa mwaka 2006 kama ulivyoelezwa katika hotuba ya Katibu Mkuu. Ukame huo uliathiri sekta ya nishati, uzalishaji wa chakula mashambani, na idadi kubwa ya mifugo na wanyama wengine kufa na hivyo kuathiri uchumi na maisha ya binadamu.

Kutokana na hali hiyo, na kwa kuzingatia umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji, Serikali, kupitia tamko la Mheshimiwa Makamu wa Rais, ilitangaza Mkakati wa Hifadhi ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Mkakati huo una uhusiano mkubwa na utunzaji, usimamizi na matumizi ya rasilimali za maji nchini. Hivyo basi, ni vema tukajikumbusha changamoto 12 zilizoainishwa katika mkakati huo.

Changamoto Na. 1: Uharibifu wa mazingira utokanao na uvamizi wa wafugaji kwenye maeneo ya vyanzo vya maji.

Changamoto 2: Uharibifu wa mazingira kutokana na uvamizi wa shughuli za kilimo kwenye miteremko ya milima, mabonde na vyanzo vya maji.

Changamoto 3: Uharifibu wa mazingira utokanao na ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa na ujenzi wa nyumba mijini.

Changamoto 4: Umwagiliaji usiokuwa endelevu unaosababisha kutoweka kwa bioanuawai na upungufu wa maji ya kuendeshea mitambo ya kuzalisha umeme.

Changamoto 5: Ukosefu wa kumbukumbu/ takwimu sahihi na za kutosha kuhusiana na vyanzo vya maji na kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi na maendeleo wilayani.

Changamoto 6: Uharibifu wa mazingira na wa vyanzo vya maji utokanao na moto.

Changamoto 7: Kukauka kwa vyanzo vya maji kutokana na kupanda aina ya miti inayotumia maji mengi.

Changamoto 8: Kuenea kwa hali ya jangwa na ukame katika maeneo mengi nchini.

Changamoto 9: Uelewa na ushiriki mdogo wa wananchi katika hifadhi ya mazingira.

Changamoto 10: Migongano katika matumizi ya ardhi baina ya wadau mbalimbali na uharibifu wa mazingira.

Changamoto 11: Uharibifu wa mazingira utokanao na shughuli za uchimbaji madini.

Changamoto 12: Uchafuzi wa mazingira utokanao na taka za plastiki.

Ndugu Wajumbe, naamini kwamba katika kuweka mfumo wa kutathmini maendeleo ya usimamizi wa rasilimali za maji, mtanzingatia hifadhi ya vyanzo vya maji na rasilimali maji kwa ujumla na kuandaa vigezo au viashiria vitakavyowezesha kujipima katika eneo zima la hifadhi ya mazingira.
Naamini pia mmehusika katika maandalizi ya mkakati wa hifadhi ya mazingira ya bahari, maziwa, mabwawa makubwa na maeneo yanayaozunguka bahari, maziwa na mabwawa makubwa. Rasimu ya Mkakati huu bado inapitia ngazi mbalimbali za kiserikali. Mkiwa wadau wakubwa wa maeneo ya rasilimali hizi bila shaka mtajihusisha kikamilifu katika utekelezaji wa mkakati huo, utekelezaji ambao utaratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

3. Madhumuni ya Mkutano

Ndugu Wajumbe, mkutano huu utapokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Mabonde na mada mbalimbali zitakazowasilishwa ambazo zinalenga maudhui ya mkutano wa mwaka huu. Taarifa hizo za kila Bonde zitaelezea mafanikio na changamoto za utekelezaji katika usimamizi wa rasilimali za maji nchini, hifadhi ya mazingira na vyanzo vya maji, kujenga uwezo wa watumishi, uimarishaji wa kitaasisi na usimamizi wa sheria zinazohusu hifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji.
Mkutano huu pia utapata maelezo juu ya uzoefu wa Bonde la Mto Pangani na Mto Wami/Ruvu katika utekelezaji wa Programu ya Tathmini ya Mahitaji ya Maji kwa ajili ya Mazingira (*Environmental Flow Assessment*) na uzoefu wa usimamizi wa pamoja wa rasilimali za maji kitaifa na kimataifa.

Ndugu Wajumbe, ni matarajio yangu kuwa baada ya mkutano huu na kwa kupitia taarifa na mada zitakazowasilishwa, madhumuni ya mkutano huu yatakuwa yamefikiwa. Madhumuni hayo ni pamoja na:-

- Kubadilishana uzoefu na uelewa juu ya dhana ya usimamizi na matumizi bora na endelevu ya rasilimali za maji kwa kufuata mfumo wa Mabonde.

- Kuweka utaratibu wa kuziwezesha Bodi za Maji za Mabonde kufanya tathmini ya usimamizi wa pamoja wa rasilimali za maji.
- Kuelimishana juu ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ya mwaka 2006 - 2025 hususan Programu Ndogo ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji.
- Kuimarisha uwezo wa kimfumo na kitaasisi katika kusimamia rasilimali za maji kwa maendeleo ya taifa.

Matokeo ya mkutano huu yatachochea utekelezaji wa malengo mbalimbali ya Sekta ya Maji. Ninatarajia kuwa mtatumia mbinu na uzoefu mtakaoupata katika kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa njia ya usimamizi wa pamoja.

Ndugu Wajumbe, nimefarijika sana kusikia kwamba fedha za utekelezaji wa Programu hii zimekwishatolewa na kufika katika ngazi za Mabonde. Hivyo, ni matarajio yangu kwamba mtatekeleza majukumu yenu kama yalivyoainishwa katika Mkataba kati ya Wizara na Bodi zenu na kutoa taarifa ya utekelezaji kulingana na taratibu zilizomo katika Mkataba huo. Wizara inayo matumaini makubwa kwenu, hususan katika kuweka miongozo imara itakayofanikisha utekelezaji wa majukumu yenu kama yalivyoainishwa katika makubaliano. Napenda kuchukua nafasi hii kuwakumbusha kwamba uhai, uchumi na maendeleo ya taifa hili yanategemea upatikanaji na matumizi ya maji yenye tija.

4. Rasilimali za Maji katika Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Maji

Kama mnavyofahamu, Serikali tayari imepitisha na imeidhinisha kwa ajili ya utekelezaji **Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Maji.** Mkakati unaainisha maeneo na mambo muhimu ya kufanya katika kuendeleza na kusimamia rasilimali za maji, huduma za maji safi na majitaka, na uimarishaji wa vyombo na asasi zinazohusika. Mkakati pia umeanisha majukumu ya wadau mbambali, kazi za kutekelezwa, watekelezaji na muda wa utekelezaji.

Kuhusu usimamizi wa rasilimali za maji, malengo ya mkakati yanahusu, pamoja na mambo mengine:

- Kuweka muundo wa kitaasisi utakaotuwezesha kuwa na matumzi endelevu ya rasilimali za maji, na
- Kuimarisha ushirikiano wetu na mataifa mengine katika kusimamia matumizi ya maji shiriki.

4.1 Muundo wa Kitaasisi

Ndugu Wajumbe, kuhusu muundo wa kitaasisi, mkakati unaongozwa na malengo ya Sera ya Maji ambapo tunatakiwa kuhakikisha kwamba "**Vyombo vya kusimamia maji kimabonde vinatekeleza majukumu yake na panakuwepo na uhuru wa kufanya maamuzi yake na kujiendesha vyenyewe kimapato"**. Lengo la kujiendesha kimapato ni muhimu likapewa uzito katika mikakati ya kuendeleza Mabonde. Kuhusu uhuru wa

kufanya kazi, niseme tu kwamba hakuna uhuru usio na mipaka. Mipaka ya uhuru huo ni sheria za nchi, tarabitu zitokanazo na sheria hizo, na kanuni za kazi zitakazowekwa na Bodi za Mabonde. Ndani ya mipaka hiyo, Serikali itaheshimu na kusimamia uhuru huo, ikizingatiwa kwamba tofauti na rasilimali nyingine, rasilimali maji zinahusu uhai na usalama wa nchi.

Suala jingine linalowahusu na linalohusu muundo wa kitaasisi ni uamuzi wa Serikali wa kuundwa upya kwa Bodi ya Taifa ya Maji. Chombo hiki kitakuwa na jukumu la kumshauri Waziri mwenye
dhamana ya maji kuhusu masuala ya sera na utekelezaji wa Sera ya Maji, na masuala ya kitaifa na kimataifa yanayohusu usimamizi, uendelezaji na matumizi ya rasilimali za maji. Chombo hiki vile vile kitahusika na kuratibu shughuli za Bodi za Maji. Mfumo huu utapunguza la ongezeko idadi ya taasisi na hivyo kupunguza mzigo kwa Serikali.

4.2 Ushirikiano wa Kimataifa

Tumebahatika kama nchi kuwa na nchi jirani nane zinazotuzunguka. Kutokana na bahati ya jiografia hii tunayo mabonde shirikishi ya maji. Mabonde hayo shirikishi ni pamoja na **Bonde la Nile; Bonde la Zambezi; Bonde la Ruvuma** na **Bonde la Pangani,** yakihusisha mabonde yetu ya Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, mto Ruvuma na mto Pangani.

Sera ya Maji ya mwaka 2002 inasisitiza umuhimu wa kuendeleza ushirikiano wa kimataifa katika kupanga na kusimamia matumizi ya rasilimali za maji. Kwa kuwa mabonde shirikishi yanahusisha rasilimali za maji za kimataifa, tunapotekeleza azma yetu ya kuwa na
mfumo wa kutathmini maendeleo ya utekelezaji wa rasilimali za maji nchini, inatubidi tuwe na viwango vya kimataifa vinavyoweza kueleweka na kutafsirika vizuri baina ya nchi zinazohusika. Changamoto iliyo mbele yetu ni kukumbuka kwamba kazi tunayoifanya ituwezeshe pia kuendeleza ushirikiano wa kimataifa.

5. Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji

Sera ya Maji inatutaka tuwe na mfumo madhubuti wa kisheria wa usimamizi wa rasilimali za maji. Hivi sasa sheria mama inayosimamia matumizi ya rasilimali za maji ni Sheria ya Matumizi ya Rasilimali za Maji, Na. 42 ya mwaka 1974. Sheria hii imefanyiwa marekebisho mwaka 1981, 1989 na 1999, na kanuni zake zilirekebishwa mwaka 1975, 1994, 1996 na 1997. Sheria hii haikidhi mahitaji ya wakati uliopo. Ili tuweze kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Maji kwa ufanisi zaidi, inabidi sheria hii ifutwe. Hivi sasa tunaandaa rasimu ya muswada wa sheria ya Rasilimali za Maji. Kwa upande wa utoaji huduma ya maji, tunaandaa vile vile rasimu ya muswada wa Sheria ya Huduma za Maji.
Ombi langu kwenu ni kwamba pindi Serikali itakaporidhia maandalizi ya miswada hii, mhusike kikamilifu katika mijadala itakayokuwepo, kwa nia ya kuelewa kwa undani na

kuboresha, ikibidi. Hii itakuwa ni moja ya nyenzo zenu muhimu za kutekelezea majukumu yenu.

6. Hitimisho

Ndugu Wajumbe, usimamizi madhubuti wa matumizi ya rasilimali za maji katika sekta zote za kiuchumi na kijamii unahitajika ili kuleta tija. Kwa upande wa Ofisi za Mabonde, kila Bodi ina wajibu wa kuhakikisha kuwa inabuni mbinu na mikakati sahihi ya kukabiliana na hali hii. Wadau wakubwa katika kazi zenu ni watumiaji maji na wananchi walio katika mabonde yenu. Ni jukumu kubwa lakini muhimu kwa Bodi zenu kuwaelimisha kuhusu kutumia maji kwa busara, uangalifu na kwa tija. Kwa upande wetu na kwa kushirikiana nanyi, tutaendelea kuboresha utaratibu wa ugawaji wa maji kwa haki na usawa kwa lengo la kunufaika na fursa zilizopo katika sekta zote za kijamii na kiuchumi.

Huu ni mkutano wa kwanza unaonihusisha mimi na Bodi za Mabonde yetu yote tisa. Lakini huu vile vile ni mkutano wenu wa kwanza. Kwa maana hiyo mimi pamoja nanyi wote ni wageni katika mikutano kama hii. Mkutano wa kwanza una changamoto moja kubwa ; kuweka msingi wa mafanikio yake na mafanikio ya mikutano inayofuata.

Nilianza kwa kuelezea umuhimu wa kutunza rasilimali za maji kupitia, pamoja na njia nyingine Mkakati wa Hifadhi ya Ardhi na Vyanzo vya Maji; nimeelezea pia madhumuni ya mkutano huu ; nimejaribu kwa kifupi kufafanua masuala ya kimkakati na kisheria yanayohusu rasilimali za maji, na kuwasihi mhusike kikamilifu katika maandalizi ya awali ya miswada ya sheria mpya. Pale ilipowezekana nimetoa changamoto ambazo mnaweza kuzitafakari zaidi.

Nahitimisha kama nilivyoanza kwa kuwashukuru wote mliohudhuria. Kwa niaba ya Serikali, nawashukuru sana wahisani au washiriki

wenzetu katika sekta ya maji. Nawashukuru wale wote mliohusika na maandalizi ya mkutano huu ambao ni wa ki-historia.

Baada ya kusema hayo, naona fahari kutamka kwamba Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Maafisa wa Maji wa Mabonde, umefunguliwa rasmi.

‘Maji ni Uhai’

Asanteni sana kwa kunisikiliza.